

MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI SEPTEMBER, 2026 NA MWELEKEO KWA MWEZI OKTOBA, 2026.

Dondoo za tathmini ya Septemba, 2026 na mwelekeo wa Oktoba, 2026:

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Septemba, 2026 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto kwa mwezi Oktoba, 2026 nchini.

- i. Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2026 maeneo mengi nchini yaliendelea kupata vipindi vya baridi ya wastani, hususan nyakati za usiku na asubuhi.
- ii. Vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Septemba 2026, hususan ukanda wa pwani, kanda ya kati pamoja na maziwa makuu. Aidha, vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani, ukanda wa ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na nyanda za juu kusini magharibi.
- iii. Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2026, mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, mvua za Juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo hayo.


1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBER, 2026.

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2026 hali ya ukavu ilijitokeza katika maeneo mengi ya nchi iliyoambatana na hali ya baridi ya wastani kwa baadhi ya maeneo, hususan nyakati za usiku na asubuhi. Kiwango cha chini kabisa cha joto cha nyuzi joto 7.6 kiliripotiwa katika kituo cha Igeri (mkoa wa Njombe) mnamo tarehe 7 Septemba, ikifuatiwa na nyuzi joto 7.6°C katika kituo hicho tarehe 4 Septemba 2026.

Vipindi vya upepo mkali unaofikia kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ukanda wa pwani, maziwa makuu na kanda ya kati. Aidha, vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na nyanda za juu kusini magharibi. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 43.6 kilirekodiwa katika kituo cha hali ya hewa Pemba mnamo tarehe 18 Septemba, 2026.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanga Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz



Kielelezo 1: Viwango vya joto la chini kwa vituo vya Uyole na Igeri katika mwezi Septemba, 2026.

2.0 MWELEKEO KWA MWEZI OKTOBA, 2026

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la Bahari katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, ikiashiria kuanza kuimarika kwa hali ya El Niño. Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi, karibu na Pwani ya Afrika mashariki, linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, wakati eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la bahari la chini kidogo ya wastani hadi wastani. Hali hii inatarajiwa kuongeza upepo wenye unyevu kuvuma kuelekea ukanda wa pwani ya nchi yetu na mikoa ya jirani. Joto

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki, karibu na pwani ya Angola linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani hadi wastani.

Kwa upande mwingine, joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (kusini mwa kisiwa cha Madagascar) linatarajiwa kuendelea kua la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kudhoofisha mgandamizo mkubwa wa hewa wa Mascarene na hivyo kupunguza kasi ya upepo wenye baridi unaovuma kutoka kusini kuelekea katika maeneo ya nchi yetu.

2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2026

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2026, mvua za msimu wa Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi.

Kwa upande mwingine, hali ya joto kiasi inatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan ukanda wa pwani wa nchi. Vilevile, vipindi vya baridi ya wastani vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu Kusini magharibi pamoja na kusini mwa nchi hususan nyakati za usiku na asubuhi.

Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne kwa baadhi ya maeneo haya.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne kwa baadhi ya maeneo haya.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo za radi katika maeneo machache vinatarajiwa. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu kwa baadhi ya maeneo haya.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):

Maeneo haya yanatarajiwa kua na vipindi vichache vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache hususani katika wiki ya tatu na ya nne.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):

Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):

Vipindi vya mvua nyepesi zitakazoambatana na baridi ya wastani vinatarajiwa hususan nyakati za usiku na alfajiri.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):

Vipindi vifupi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususani kuelekea mwishoni mwa mwezi.

2.3 MATARAJIO KWA MWEZI NOVEMBA, 2026

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2026 mvua za Vuli zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

2.4 USHAURI

Tahadhari za kiafya zichukuliwe ili kulinda jamii dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na baridi, vumbi na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi katika kipindi hiki, maji na malisho yanapaswa kutumika kwa uangalifu ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendeleo kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

Imetolewa tarehe 01 Oktoba, 2026 na:

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz